

- Mingine inaweza kuhimili maji mengi kama vile *Marawa*, (*Mutangauzi*), *Kihua* (*Brugmansia*), na *Mugagatio*.
- Mingine kama *Mugagatio* inaweza kuhimili asidi katika mchanga tofauti na mmea kama *Lucerne* unaositishwa kukua na asidi nyingi.
- Mingine huhimili kiangazi kikubwa kama vile *Mugumo*, *Grewia*, *Mukuriundu*, *Kithunju*, *Rweja Nkuti* na *Mukururu*.
- Mingine kama *Tethonia*, *Mutundu*, *Mukuu*, lantana na *Mugio* huimarisha rutuba.
- Mingine ina kiwango fulani cha dawa kwa mifugo iikulayo.



### Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P 57811, NAIROBI.  
 Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344  
 Barua pepe: resource.centre@kari.org  
 Tovuti: www.kari.org

**Mtayarishaji:**  
 Kangara, J

**Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:**

**Mkurugenzi wa Kituo,**  
 KARI-Embu

S.L.P. 27 Embu, Kenya  
 Simu: 068 2011/20873  
 Nukulishi: 068 30064

Barua pepe: kariembu@salpha.co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 11 /2008

**Shilingi 20 za Kenya**

## Tumia mimea ya kiasili kwa kulisha mifugo



## Utangulizi

Kuwalisha mifugo kwa mimea ya chakula cha mifugo ya kiasili ni mtindo wa mkulima wa kawaida. Juhudi haba zimetwa kuilima mimea hii kwa sababu ya ukosefu wa ujuzi kuhusu virutubishi vyake na utunzaji. Mimea hii inaweza kukuzwa mashambani ili kuboresha mazao ya mifugo.

## Ukuzaji

Chakula cha wanyama cha kiasili hupatikana kwenya kingo za mito, misitu, kandokando za barabara pamoja na mashamba yasiyolimwa kwa muda.

Mimea hii huendelea kukua msimu hadi msimu na ikitunzwa vizuri, virutubishi vyake vinaweza kuzidi vile vya nyasi ya kizungu na mimea mingineyo ya kigeni.



Kihua



Mutei



Mutundu

## Viwango vya virutubishi

Mimea ya kiasili			Mimea ya kigeni		
Jina	% Protini	% kus*	Jina	%	%
				protini	kus*
Mugagatio	34.8	86	Nyasi	7-12	50-64
Aborea sp	32.6	89	Likena	26	60-65
Mutundu	31.9	78.5	Sesbania	23	65-77
Mutoro	28.9	75.5	Desm	15-20	53
Mukinduri	27.8	63.3	Gliricida	20-23	74
Munoria Nthenge	26.3	70.0			
Mukuu	25.2	64.7			
Mutei	19.0	72.9			
Mukeu	24	72.1			
Mutare	23.8	89.9			
Muthara	22.8	65.8			
Muthuana	18.5	67.6			
Muthiriti	18.1	65.6			
Mutheregendi	17.6	66.8			
Muuti	17	71.8			
Muthatha	16.9	66.8			

## Manufaa ya ziada

Chakula cha mifugo cha kiasili kina faida zingine zinachokifanya kuwa mwafaka kwa mkulima mdogo. Hizi ni pamoja na:

- Mimea kama Mutundu, Mukwego, Mugumo na Mtare hukua katika mazingira mengi tofauti ya kilimo.